

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA THELATHINI NA TATU

30 MEI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA THELATHINI NA TATU – TAREHE 30 MEI, 2022

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO
WA AFRIKA MASHARIKI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA
BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya


Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

283. MHESHIMIWA DEUS CLEMENT SANGU (KWELA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-



Je, ni lini ujenzi wa barabara inayounganisha Mji Mdogo wa Mtowisa na Sumbawanga Mjini kuititia Mlima Ng'ongo utaanza.

284. MHESHIMIWA DKT. DAVID MATHAYO DAVID (SAME MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kwa nini Serikali haitengi fedha za TARURA kwa kuzingatia jiografia, ukubwa wa eneo na mazingira ya Wilaya au Jimbo husika.

285. MHESHIMIWA GRACE VICTOR TENDEGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itawapa mafunzo Maafisa Masuuli na Wahasibu wa Halmashauri juu ya uandaaji wa taarifa za ukaguzi wa fedha.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

286. MHESHIMIWA JUSTIN LAZARO NYAMOGA (KILOLO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, ni lini Serikali itaomba fedha za Mifuko ya Kupunguza Hewa ya Ucaa Duniani na kuwalipa Wananchi wanaotunza misitu Kilolo.

WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

287. MHESHIMIWA DKT. OSCAR ISHENGOMA KIKOYO (MULEBA KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, ni lini Serikali itajenga minara ya simu katika Kata za Karambi, Mubunda, Ngenge na Rutoro katika Wilaya ya Muleba.

WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:

288. MHESHIMIWA DKT. CHARLES STEPHEN KIMEI (VUNJO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Soko la Kimataifa katika eneo la Lokolova mpakani mwa Tanzania na Kenya.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**289. MHESHIMIWA SHALLY JOSEPHA
RAYMOND (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, nini mpango wa kuweka mazingira wezeshi ya kupata mbegu bora za malisho kama Luseni na kuwezesha uzalishaji wa Mitamba.

WIZARA YA NISHATI:

**290. MHESHIMIWA IDDI KASSIM IDDI
(MSALALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itaanzisha Mkoa wa TANESCO katika Wilaya ya Kahama na kujenga Ofisi ya TANESCO ya Halmashauri.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

- 291. MHESHIMIWA DKT. FLORENCE GEORGE SAMIZI (MUHAMBWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itatoa Vitambulisho vya NIDA kwa Wananchi wa Mkoa wa Kigoma hususan Jimbo la Muhamwe.

- 292. MHESHIMIWA JACKSON GEDION KISWAGA (KALENGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itajenga Vituo vya Polisi katika Mahakama za Kata nchini.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

- 293. MHESHIMIWA REUBEN NHAMANILO KWAGILWA (HANDENI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Handeni Kibirashi, Kondoa hadi Singida kwa kiwango cha lami.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

DODOMA
30 MEI, 2022

N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE